# *Waebrania, Mlango Wa Pili* [1]

Tulikuwa hapa darasani na kufurahia ninii... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Na sasa kitabu cha kwanza cha Waebrania, ni Paulo, tuliona, ama tunaamini. Wanatheolojia wameshindwa; hawajui kabisa ni kipi, ama ni nani aliyekiandika. Lakini, ninaamini, mtu yeyote aliye na utambuzi mdogo wa kiroho angeweza kuona ilikuwa ni Paulo. I—inaaminiwa, na karibu waandishi wote, kuwa ni Paulo. Na jinsi ambavyo alininii...

2 Katika mlango wa 1, tuliona ya kwamba ilikuwa ni kumtukuza Bwana Yesu. Loo, jinsi alivyolileta, kuonyesha kwa—kwa ujuzi aliokuwa nao akienda zake Dameski. Sasa, Paulo alikuwa, hapo mwanzoni, mwanatheolojia halisi. Paulo alifundishwa chini ya Gamalieli, mmoja wa waalimu walio bora sana wa siku hizo. Naye alikuwa ni msomi na mwenye akili, naye alikuwa ni mwalimu hodari sana wa Biblia.

3 Nami niliona jambo hili, wakati alipokuwa njiani akienda zake Dameski, akiwa na barua mfukoni mwake, apate kuwatia mbaroni wote wale waliokuwa kwenye njia ya Injili Takatifu ya zamani za kale iliyobarikiwa, na mtu huyo alikuwa ni mwaminifu. Lakini, daima nimeamini ya kwamba tangu Paulo alipomwona Stefano akifa, nafikiri jambo hilo hapana budi lilimkera sana. Wakati aliporidhia kifo cha Stefano, na akashika makoti ya hao waliompiga mawe, basi Paulo alikuwa na hatia ya damu ya Stefano. Naye alikiri, na kusema, "Hata sistahili," kasema, "kwa maana nilimwaga damu ya nanii Wa—Wake, mfia imani, Stefano. Maana, yeye aliyashuhudia hayo.

4 Na kama ukishuhudia chochote, wewe una hatia tu kama kuwa mshiriki wake. Kwa hiyo kama tukishuhudia, tuseme, "Loo, naam, hawakupaswa kufanya jambo hili, jambo hili *fulani*." Kuwa mwangalifu na yote unayosema, kwa maana una hatia jinsi hukumu yako inavyoelekea. Kama huwezi kuamua, usiseme kitu, liache tu. Basi unapokiri ya kwamba wewe ni Mkristo, basi una hatia. Unaona? Una hatia ya kuwa Mkristo, nawe huna budi kuuishi huo. Na Mungu anapotoa a—ahadi katika Biblia...Ninamwona mtu hapa kwenye kiti cha magurudumu. Mungu anapofanya ahadi, Yeye ana hatia kwa ahadi hiyo isipokuwa iwe anaitimiza. Mungu ana hatia anapofanya Ahadi. Na Maandiko yana hatia mpaka yatakapotimizwa. Unaona? Yako—yako hapo kwa kweli kama ta—kama tamshi ambalo Mungu amefanya. Nalo halina budi kutimizwa la sivyo Mungu ana hatia. Unaona?

5 Na kwa hiyo Paulo, akiwa ni mwalimu, na akishuka njiani kwenda zake Dameski siku hiyo, yapata, yapata saa

sita za mchana, nadhani. Kulikuwa na Nuru kuu iliyoangaza kutoka Mbinguni, nayo ilimpofusha, naye a—akaanguka ardhini. Naye akasema alitaka kujua Huyo alikuwa ni nani. Alisema sauti ilinena, na kusema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?” Ninaamini mlango wa 8 wa Matendo.

Akasema, “Ni nani huyo ninayemwudhi?”

6 Ndipo hiyo sauti ikarudi, na kusema, “Mimi ni Yesu.” Loo! “Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo.” Basi Yesu alikuwa ni nini wakati huo? Yesu, Yeye alikuwa ni Nuru, Nuru kubwa tu inayong’aa sana.

7 Sasa ili kututia moyo na kupata msingi hapa. Yeye alikuwa ni Nuru kwa namna gani, ambapo alikuwa ni Mwanadamu? Sasa, hakuna mtu . . .

Kulikuwako na kundi la askari waliokuwa pamoja na Paulo, walinzi wa hekalu, wakishuka kwenda kuwatia mbaroni. Paulo alikuwa ndiye jemadari mkuu. Nao walikuwa wakishuka kwenda kuwakamata hao watu, kwa ajili ya kampeni zao na kadhalika, na kwa ajili ya tumaini lao la kidini lililokuwa ndani yao.

8 Lakini, sasa, huyu hapa Yesu kama Nuru kubwa. Sasa, kama ukikumbuka, hapo mwanzo, Yesu alikuwa ni Nuru. Yesu alikuwa ni Logos iliyotoka kwa Mungu. Naye alikuwa ni ninii . . . Alikuwa ni Malaika wa Agano ambaye aliwaongoza wana wa Israeli nyikani. Naye alikuwa ndiye ile Nguzo ya Moto walioyoitazama. Naye alikuwa . . . Na wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu, Nami ninarudi kwa Mungu.” Kwa hiyo kama Yeye alitoka kwenye Nguzo ya Moto, akawa Mwanadamu, basi kama alirudi mahali alikokuwa, alirudi akawa ni Nuru tena. Naye alikuwa ndiye huyo hapo wakati Paulo alipomwona, Yeye alikuwa ni Nuru.

9 Sasa, hao askari wote waliokuwa pamoja na Paulo hawakuiona ile Nuru. Basi inawezekana ya kwamba mtu anaweza kuiona na hao wengine hawataiona? Hakika. Vema. Yeye, Paulo, aliiona, bali hao wengine hawakuiona hiyo Nuru..

10 Sasa, wakati Petro alipokuwa gerezani, tunaona ya kwamba Nuru hii iliingia gerezani, ikaifungua milango. Naye alikuwa . . . Nuru hiyo iliwapofusha hao walinzi wengine, walipokuwa wakitoka, Petro akiondoka. Na alipofika mlangoni, ulijifungua tu wenyewe, kimya kimya, ukajifunga nyuma yake. Kutoka katika gereza la ndani, akaenda kwenye mlango wa nje. Ukajifungua wenyewe, ukajifunga kimya kimya. Na halafu akaenda kwenye pengo, akatoka akaingia kwenye barabara ya mji. Ndipo akasugua macho yake, kana kwamba kusema, “Hivi nilikuwa nikiota?” Hakujua nini kilichokuwa kimetukia. Lakini, Malaika wa Bwana, Malaika yeye yule aliyekuwa Nguzo ya Moto iliyomwongoza Musa hadi baharini na kuifungua, loo, na Bahari

ya Chumvi . . . Bahari ya Shamu ilifanya ukuta pande zote mbili, nao Israeli wakavuka.

11 Na walipofika kwenye Yordani iliyofurika, Yeye hakujionyesha Mwenyewe wazi pale. Lakini alikuwa yupo pale, maana aliifungua tu. Nao walivuka katika mwezi wa Aprili, wakati nyanda hizo zote zimejaa maji. Naye akazuia chemchemi, na akazuia barafu isiyeyuke, maana hayakuendelea kufanya ukuta mrefu kwenda juu zaidi na zaidi; yalisimama tu. Huyo ni Yehova wetu. Huyo ni Bwana wetu Yesu. Yalisimama tu; nao wakatembea wakavuka katika nchi kavu.

12 Sasa, Mungu aliahidi ya kwamba Yeye angewaangalia, kwa hiyo Yeye aliwajibika kwa ahadi Yake. Sasa, Paulo, akijua mambo haya, na akiyajua, alipata heri, kwa maana Mungu alikuwa akizungumza moja kwa moja na Paulo. Hakuwa akizungumza na wale askari waliokuwa pamoja naye. Alikuwa akizungumza na Paulo tu.

13 Sasa, wakati Ma—wakati Malaika wa Bwana aliposhuka, katika umbo la nyota; nao wale wanajimu, wale mamajusi wa India, wakati, walipoiona hiyo Nyota na wakaifuata kwa mamia ya maili. Nayo ilipitia juu ya kila kituo cha utafiti wa anga, maana wao waliangalia wakati kwa nyota. Wala hakuna aliyeiona hiyo Nyota ila wale mamajusi. Loo, jamani! Hivi hilo haliwasisimui? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

14 Kwa hiyo, unaona, Mungu hashughuliki na madhehebu. Hashughuliki na makundi ya watu. Yeye hushughulika na watu binafsi. Yeye hujifunua Mwenyewe kwa watu binafsi. Na sasa—sasa kusema jambo hili, si hili . . . Mungu anajua moyo wangu. Wala si kusema jambo hili kwa nafsi yangu mwenyewe, kujisifu binafsi, sasa; kuwa tu pale. Bali, hivi ulijua, Mungu yeye huyo, Yesu yeye huyo, yupo pamoja nasi asubuhi ya leo. Je! unajua, kila mmoja wenu ana ushuhuda mdogo, wa kibinafsi wa jambo hilo sasa hivi, ya kwamba Yeye yupo hapa? Na ananinii . . . Ametufanyia jambo fulani katika siku hii ambalo hakufanya katika siku hizo nyingine; Yeye amepigwa picha Yake siku hizi. Tunayo imening'inia moja kwa moja *pale*. Unaona? Ile Nguzo ya Moto, Bwana Yesu yule yule.

15 Angalia jinsi Yeye anavyofanya kazi wakati huu wa sasa. Kama Yeye ni Bwana Yesu yule yule, Yeye atafanya mambo yale yale, kwa kuwa Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

16 Sasa, kabla Paulo hajatangaza jambo lolote, kama hili lilikuwa ni kweli ama si kweli, kwanza alishuka akaenda Misri na akakaa miaka mitatu kule, apate kujua kama lilikuwa ni la Kimaandiko ama hapana. Je! Ulipata kujua jambo hilo? Baada ya kuongoka kwa Paulo, yeye alishuka akaenda Misri kwa muda wa miaka mitatu. Akakaa huko, na huko ndiko alikojifunza hekima hii kuu.

17 Sasa, si kwa kujilinganisha hata kidogo, ninawaelezea tu jinsi ambavyo Roho Mtakatifu angali anadumu yule yule. Sasa, kanisa langu hapa linakumbuka, miaka kadhaa iliyopita, wakati Malaika huyu angetokea na angeonyesha mambo. Mimi nilishuku jambo hilo kidogo. Ninyi nyote mnajua jambo hilo, ninyi watu wa zamani. Kama ninyi . . . Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, wakati mmesikia. Naam. Angalia, angalia kanisa, lililosalia, kutoka kwa hao watu wa zamani. Unaona? Nilishuku, kwa sababu wahubiri waliniambia Huyo alikuwa ni wa Ibilisi. Nami kwa namna fulani niliamini jambo hilo, bali nilingojea. Nisingesema chochote juu yake.

18 Lakini, loo, Jina la Bwana libarikiwe! Usiku mmoja, mahali fulani pale, Yeye alishuka, Malaika, na akalifunua katika Maandiko, ya kwamba ilikuwa ni Yeye. Na nilipoliona katika Maandiko, basi kuulipua Huo ulimwenguni kote, huo Ujumbe.

19 Kutokana nao wametokea hapo akina Oral Roberts, A. A. Allen, Tommy Osborne, Tommy Hicks, na kadhalika. Unaona? Ni Ujumbe kwa watu.

20 Na Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kimaandiko, ni yeye yule. Anatenda vile vile. Ni yeye yule. Naye hutenda vile vile. Hujidhihirisha vile vile. Naye yupo hapa, asubuhi ya leo, yeye yule. Sasa tunaweza tukamwona; tunaweza tusimwone. Chochote kile, tuna ushuhuda sasa hivi ya kwamba Yeye yupo hapa.

21 Sasa, tunaona sasa ya kwamba, Paulo, kwa tukio hili, na akiandika nyaraka hizi, karibu zote, kutoka gerezani, alikuwa amelinganisha Agano la Kale na Agano Jipya. Sasa kumbuka, mwandishi wa mwisho wa Biblia hii, kwa uvuvio, Mungu alishuka chini na kumwambia, "Mtu yeyote akiongeza lolote Kwake au akiondoa lolote Kwake, sehemu yake itaondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima, kumhusu yeye." Kwa hiyo tusithubutu kuongeza jambo moja Kwake. Loo, halina budi kudumu jinsi lilivyo, halipaswi kuongezewa chochote. Nasi tunapaswa kushindania kila kitu kilicho ndani Yake. Mimi sitaki cha zaidi, wala sitaki chochote pungufu. Ninataka yale tu kisemayo.

22 Sasa, Kitabu hiki cha Waebrania, sababu ya mimi kukichagua; kusudi moja, jambo moja; waraka huu, "Mpendwa Ndugu Branham," na kadhalika. Na, mimi—mimi, tunataka kudumu na Neno.

23 Sasa, mlango wa 1, ulikuwa unamtukuza Yesu, kwa hiyo Yeye ndiye muhimu. Naye Paulo alitufahamisha, hivi majuzi usiku, ya kwamba Yeye alikuwako hapo kwenye ule mwanzo mkuu. Nasi tuliona ya kwamba hakuwa kitu pungufu ya "Melkizedeki, Mfalme wa Salemu," Yule Mkuu wa mlango wa 7.

24 Na sasa, asubuhi ya leo, tunamkaribia kutoka kwenye mwingine, msimamo mwingine, kutoka kwenye mlango wa

2. Sasa, baada ya Paulo kutupa sisi Ujumbe huu mkuu na wa ajabu, wa kumtukuza Yesu, "Na hata aliwafanya Malaika kumwabudu." Nami nafikiri, hapa, kama utaratibu ule wa mifano ya kale, "Naye ataikunja kama vazi, lakini hivyo vitaangamia, bali Wewe unadumu."

25 Na kwenye mlango wa 2, kifungu cha 2, ninaamini ndicho, "Siku hizi amesema na sisi kwa Mwanawe." Pia, angalia, "Sehemu nyingi na kwa njia nyingi Yeye alisema katika manabii." Tulipitia hayo na tukaona manabii walikuwa ni nani, na jinsi ambavyo Mungu alileta Ujumbe Wake katika manabii. "Lakini katika siku hii ya mwisho Yeye amesema katika Mwanawe, Yesu, kwa Roho Mtakatifu. Alisema katika manabii, zamani." Kisha tukarudi nyuma na tukaona, manabii hao wote walikuwa na Roho wa Kristo ndani yao.

26 Tulirejea kwa Yusufu na tukaona ya kwamba yeye alikuwa mfano kamili wa Kristo. Tulirudi kwa Musa na tukaona alikuwa ni mfano kamili wa Kristo. Ndipo tukashuka tukaja basi hata kwa Daudi. Na wakati Daudi alipokataliwa huko Yerusalemu, bila kujua ni kwa nini, bali alipanda kilimani na kuangalia nyuma juu ya Mlima wa Mizeituni, ndipo akaulilia Yerusalemu kwa sababu alikuwa amekataliwa. Miaka mia nane tangu wakati huo, Mwana wa Daudi alikataliwa kama Mfalme, huko Yerusalemu, naye akaketi kwenye kilima kile kile na kulia. Loo, Roho wa Kristo, akishughulika na watu binafsi!

27 Sasa, Paulo anaanza, kwa kusema:

> *Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa . . .*

28 Mlango wa 2, sasa, tunaanzia.

> *Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.*

29 Loo, Mungu na alieleweshe hilo barabara kabisa katika maskani hii asubuhi ya leo. Ninaomba Roho Mtakatifu alizamishe hilo ndani sana mioyoni mwenu. "Inatupasa kuyaangalia zaidi ya yote hayo tuliyosikia." Tunapaswa kuwa tu watu wa aina gani, wakati tunapomwona yule Yehova mkuu akishuka na kufanya mambo anayofanya, na kuyaona yakilinganishwa, Andiko kwa Andiko, ya kwamba hayo ni Kweli? Nasi tunaketi hapa wakati mwingine kama dutu kwenye gogo, na kutojali tu namna hiyo. Tunapaswa kushughulika, kila dakika, tukijaribu kuwaleta watu kwa Kristo. Tunapaswa kuwa mawe yaliyo hai. Kamwe hatupaswi kuwa walegevu kama tulivyo. Tutaenda mpaka kanisani, na tutamwona Bwana Yesu akifanya jambo fulani, ama—ama akitubariki kwa njia fulani, na kisha tuta—tutatoka na kurudi na kusema, "Mkutano mzuri sana."

30 Sasa, kuhubiriwa kwa Neno, tunakufurahia, bali hilo silo jambo muhimu. Hilo silo. Haitupasi kumwabudu Bwana

mara tu baada ya kusikiliza kuhubiriwa kwa Neno, kama tunavyofanya kwa kawaida, kumwabudu tu. Hilo ni zuri sana. Lakini tunapaswa kumwabudu kila saa ya maisha yetu. Tunapokuwa kazini, tunapaswa kumwabudu. Kila wakati nafasi inapojitokeza, mwabudu Bwana kwa kushuhudia habari Zake.

Kama ukiona, baadhi yenu nyinyi akina dada, ukimwona mwanamke akiwa yuko makosani, mwabudu Bwana kwa kumchukua na kusema, "Dada, kuna maisha bora zaidi kuliko haya."

31 Ninyi wanaume kazini mwenu, mnapomsikia mtu akilitumia Jina la Bwana bure, pata nafasi uchepuke kando na uende pahala fulani, na umshike mkono, na kusema, "Wewe, kuna maisha bora zaidi kuliko haya. Haikupasi kutumia maneno hayo." Nawe umwambie kwa njia ya upole na utu wema. Mambo hayo yote ni ibada.

Na tunapomwona mtu fulani ni mgonjwa, na daktari anasema hakuna jambo lingine zaidi linaloweza kufanywa, tunapaswa kumwabudu Bwana kwa kuwaambia, "Kuna Mungu wa Mbinguni anayejibu maombi."

32 Na tena tunapoona mambo hayo yakitukia, tunayoyaona yakitukia kwa wingi, haitupasi kuyaacha mambo hayo yaponyoke. Tunayaacha tu yapitie kwenye vidole vyetu. Hiyo ndiyo shida ya kanisa kuu la Kipentekoste siku hizi. Wameachilia mambo yaliyo muhimu kuliko yote yapite kwenye vidole vyao, wakati walikuwa wameyashika mikononi mwao. Lakini, angalia yale waliyofanya, wamefanya kama hayo makanisa mengine. "Walipiga mbio bure, katika njia ya Kora, kisha wakaangamia; na njia ya Kaini, na kuangamia katika maasi ya Kora."

33 Wameunda madhehebu. Badala ya kuwa na undugu ambapo sisi sote tungeweza kuwa mmoja, wao wamejiundia madhehebu. Wakafanya mashirika madogo na itikadi ndogondogo, na wakaruka kutoka hapo na kuvunja tu undugu. Na kama msipokuwa waangalifu, Wabaptisti na Wapresbiteri watayachukua, maana, "Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Nasi tume—tumeyaacha yaponyoke kutoka mikononi kwa kufarakana.

34 Wahindi waliipotezaje nchi hii kwa mzungu? Ni kwa sababu walikuwa wametengana. Kama wangalifanya msimamo mmoja mkubwa wa mstari wa mbele . . . Bali walikuwa wakipigana wao kwa wao. Wangaliweza kushinda kama wangaliungana.

35 Tutashindwaje? Kwa sababu tumetengana. Ni jinsi gani tunavyopoteza mawasiliano yetu na Mungu, ni kwa kuwa tunatengana. Tunaunda moja, na kuliita *hili* ni Me—Methodisti, na *hili* ni Baptisti, na *hili* ni Assemblies, na *hili* Umoja, na *hili kitu kingine*, na kanisa la Mungu, na Nazarayo, na Pilgrim Holiness. Tunautenganisha Mwili wa Kristo. Hatupaswi kamwe

kutengana. Huenda tukatofautiana katika mawazo, lakini hebu na tuwe ndugu wa moyo kwa moyoni. Mungu anatutaka tuwe hivyo. Yeye alikufa kwa ajili ya Kanisa zima la Mungu. Nasi hatutaki kutengana.

> Sasa *imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.*
>
> *Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, . . .*

36 Unasikia Hilo? "Ikiwa lile neno lililonenwa na malaika . . ." Sasa, *malaika* ni "mjumbe." Neno *malaika* linamaanisha "mjumbe." Na ndiyo kwanza tumalizie, katika kitabu cha 1 hapa, "Mungu, kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, alisema na baba zetu katika manabii." Hao walikuwa ni wajumbe wa Mungu. Nao walikuwa—walikuwa ni wajumbe wa Mungu. Walikuwa ni malaika wa Mungu. Mjumbe ni malaika; ama malaika ni mjumbe, hasa.

37 Mjumbe! Wewe ni mjumbe, asubuhi ya leo. Wewe ni . . . Wewe ni mjumbe wa habari njema ama ni mjumbe wa habari mbaya. Loo, hilo si linafurahisha, kujua ya kwamba sisi ni mabalozi, ya kwamba sisi ni malaika, wajumbe wa ufufuo? Nasi ni wajumbe wa Mungu kwa ajili ya ulimwengu huu wenye dhambi, ya kwamba Kristo yu hai. Katika mioyo yetu, Yeye anaishi. Katika roho zetu, Yeye anaishi. Naye anatutoa kutoka kwenye maisha ya chini ya ufisadi ya dhambi, na kutuinua, na kutupa "haleluya" nafsini mwetu, na hutufanya viumbe vipya. Sisi ni wajumbe, malaika wa Agano. Ni jambo la ajabu jinsi gani!

38 Na sasa, katika Agano la Kale, "Ikiwa—ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara," hivyo lilipaswa kuwa ni la kweli. Katika Agano la Kale, kabla neno la nabii halijadhihirishwa, lilipaswa kuchunguzwa na kuthibitishwa. Hawakuwa wazembe nalo, kama tulivyo siku hizi.

39 Mtu anatoka tu aende zake na kuwa na namna yoyote ya mhemuko, ama chochote kile, "Loo, utukufu kwa Mungu, mambo ndiyo hayo!" Umekosea.

Biblia ilisema, ya kwamba, "Katika siku za mwisho, Ibilisi ataiga Ukristo, kwa karibu sana, hata itawapoteza walio Wateule wa kweli kama yamkini." Hilo ni kweli. Kwa hiyo, yatubidi kuujaribu.

40 Nao waliujaribu vipi katika siku zao? Kwenye Urimu Thumimu. Kile kifuko cha kifuani cha Haruni, kilichokuwa na yale mawe ndani yake: akiki nyekundu, yaspi, almasi, rubi, yakuti-samawi. Mawe hayo yote, ambayo yanawakilisha kuzaliwa kwa hawa wazee wetu kumi na wawili, yalikuwa kwenye kifuko cha kifuani cha Haruni. Na nabii alipotabiri, na hiyo Nuru takatifu iliwaka juu yake, Mungu alisema, "Hiyo ni Kweli." Lakini, haidhuru jambo lilionekana ni halisi jinsi gani

kama halikuwaka kwenye hayo, halikuwa ni la Kweli. Kwa hiyo, hizo Urimu Thumimu ziliondoka pamoja na huo ukuhani.

41 Lakini Biblia hii ni Urimu Thumimu ya Mungu siku hizi. Na wakati nabii anapotabiri, haina budi iwake kikamilifu pamoja na Biblia. Ndipo, Mungu anasema, kisha anashuka na kuthibitisha jambo Hilo.

42 Loo, jinsi ninavyoweza kumtukuza Mungu siku hizi! Ninakumbuka huko nyuma kwenye Jumapili nyingine asubuhi, iliyokuwa kama hii, nilipokuwa nikiondoka maskanini. Na ninyi watu mlikuwa mkilia na kuniomba nisiondoke. Lakini, wakati, nilipohubiri juu ya Daudi na Goliathi, na jinsi mtu utakavyokwenda kuukabili ulimwengu huo uliopoa, usiojali unaosema siku za miujiza zimepita.

43 Nilisema, "Kuna pandikizi moja kubwa la jitu, na mara tunapoweza kuliua, hao wengine watajipa moyo." Naye Bwana alitujalia hayo. Na basi kulikuwako na akina Oral Roberts na Jaggers, na kadhalika, waliovuta Upanga, nasi tukampiga adui kumtoa nchini, tukawafumba midomo yao. Hawawezi kusema kwamba miujiza haitendeki, sababu ndiyo hii hapa. Hakika. Neno la Mungu ni la Milele. Liliwaka kwenye Urimu. Likamulika kwenye Neno, hilo ndilo Urimu Thumimu Zake. Na hapo lilipowaka kwenye Hilo, ilikuwa ni kweli.

Na kwa mtu yeyote ambaye ni mhitaji, kama wewe ni mwenye dhambi, unataka kujua jinsi ya kuokolewa, "Mwamini Bwana Yesu Kristo."

44 Leo, tuna mambo mengi sana mtu unayopaswa kufanya. "Inakubidi kuanza mambo upya. Inakubidi kufanya *hivi* na kufanya *vile*, kusudi uokolewe."

Ninawazia juu ya yule mlinzi wa gereza kule Filipi, wakati mlinzi huyu alipomwuliza Paulo, "Nifanye nini nipate kuokolewa?"

Kama ingalikuwa ni wewe ama mimi, tungalimwambia mambo asiyopaswa kufanya. "Unapaswa kuacha kunywa pombe. Unapaswa kuacha kucheza kwako kamari, kucheza kwako kamari. Unapaswa kuacha jambo *hili*. *Unapaswa* kuacha *lile*.."

Paulo kamwe hakumwambia hivyo. Alimwambia tu mambo *aliyopaswa* kufanya. "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokolewa."

45 Sasa, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele." Hizo ni Urimu Thumimu zikimulika, Yohana Mtakatifu 5:14. "Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote." Yakobo 5:24, "Waite wazee, wampake mafuta, maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa." Urimu zikimulika. Unaona? Hilo ni Neno la Mungu la Milele.

46 Sijali ni washenzi wangapi, makafiri wangapi, wapagani wangapi, wenye kushuku wangapi watakaoinuka. Mungu atalitetea Neno Lake. Aliahidi atafanya jambo hilo.

47 "Na imetupasa kuyaangalia zaidi hayo tuliyosikia, tusije tukayakosa wakati wowote. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika (manabii) yalikuwa imara . . . " Je! yalikuwa imara? Tungeweza kukaa juma zima kwenye jambo hili.

48 Je! lilikuwa imara wakati Musa aliponena? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika lilikuwa imara.

Vipi kuhusu Eliya, akiketi juu ya kilele cha mlima? Bwana alimwambia, "Panda uende kule, Eliya. Nitakaa huko pamoja nawe; ninataka kufanya ushirika nawe." Mungu anapenda kufanya ushirika pamoja na watu Wake. Bali hatututulia muda mrefu vya kutosha kusudi Yeye afanye ushirika pamoja na sisi. Tuna shughuli za kurukaruka mno hapa na pale, toka mahali hadi mahali, na mambo mengi sana. "Tulia, Eliya." Yeye alitaka miaka mitatu na miezi sita ya ushirika. Sisi hatuwezi kumpa dakika tatu, ni vigumu. Miaka mitatu na miezi sita ya ushirika wa kila siku. Loo, ninapenda jambo hilo! Kasema, "Usijali juu ya kupika; tutakuwa tayari tumekiandaa. Kunguru watakulisha. Na kila kitu kitaenda kuwa sawa. Ninataka tu ushirika kidogo." Maskini nabii huyu mzee, Eliya, ameketi kule juu ya kilele cha mlima.

Wakati akiwa anafanya ushirika na Mungu, mbona, akida alisema, "Nafikiri nitapanda niende kule nikamkamate." Sasa, kamwe usijaribu kuvunja ushirika huo.

49 Kwa hiyo, akida akaja, akiwa na jeshi lake kubwa la watu, la hamsini. Na akasema, "Ni—ni—nimekuja kukuchukua, Eliya."

50 Ndipo Eliya akasimama. Angalia, huyu hapa nabii wa Bwana! Akasema, "Ikiwa mimi ni mtumishi wa Bwana, na ushuke moto kutoka mbinguni ukuteketeze." Ndipo moto ukashuka. Yule akida akasema . . .

51 "Loo, unajua nini?" Mfalme, naam, alisema, "Hiyo labda ilikuwa ni ra—radi, ni radi tu iliyokuwa ikipita, na iliwapiga. Nitatuma wengine hamsini."

52 Eliya akasimama, mmoja wa hao malaika. Neno lake ni imara. Ilibidi awe ni ujira wa haki kwa ajili ya kila kitu kilichofanywa vibaya. Akasema, "Ikiwa mimi ni mtumishi wa Bwana, na uje moto." Na hao hamsini wengine wakateketezwa kwa moto. Vema. Kila ujira!

> *Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na mwasi alipata ujira wa haki . . .*

53 Sasa, hili hapa jambo kubwa, kifungu kifuatacho.

> *Tutapataje kupona, . . .*

54 "Tutapataje kupona?" Ikiwa sauti ya Eliya ilileta maangamizi, kwa kuwa alikuwa ni malaika wa Bwana, tutapataje kupona wakati Sauti ya Kristo inaponena moja kwa moja? Ama, tunawezaje kushindwa wakati umeombewa, ikiwa ni Sauti ya Kristo? Ikiwa Kristo aliliagiza Kanisa Lake kuwaombea wagonjwa, nalo Kanisa lifanye vile alivyosema Yeye. . .kwa wao kufanya, basi linawezaje lipate kushindwa? Haliwezi. Wewe unaweza kushindwa, lakini Hilo haliwezi. Na mradi tu unalitimiza, litakuvusha.

55 Kama ukishindwa, ulishindwa wewe mwenyewe. Unaliacha tu Neno. Bali mradi tu unadumu na Neno, haliwezi kushindwa. Kwa kuwa neno la manabii lilifanya *hivi* na *vile*, ni zaidi sana vipi Neno la Kristo litakavyokuwa?

> *Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza* ulianza *kunenwa kwetu na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliomsikia yeye;*

56 Wazia jambo Hilo, lililonenwa na Bwana. Ni mara ngapi tungeweza kurudi nyuma? Tungekomea wapi, papa hapa kwa saa moja? Wakati Yesu alipokuja, ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

57 Sasa, kumbukeni, kwanza ulianza kunenwa na Yesu, Mwenyewe, na kisha ukathibitishwa na wale waliomsikia. Sasa msikilizeni.

58 Wakati alipokuja duniani, Yeye hakudai kuwa mponyaji. Yeye alisema, "Si Mimi nizitendaye hizo kazi; ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu. Ndiye azitendaye kazi hizo. Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda."Yohana Mtakatifu 5:19.

59 Angalia wakati Filipo alipomjia. Nathanaeli. . .Baada ya kuongoka kwa Filipo, aliondoka akaenda akamchukua Nathanaeli. Kasema, "Njoo, uone Ambaye tumemwona: Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

60 Ndipo akasema, "Laweza neno jema kutoka Nazareti?"

61 Kasema, "Njoo, uone." Hiyo ndiyo namna ya kushawishika: lithibitishe. Njoo uone. Loo, hilo ndilo jambo zuri sana nililopata kusikia. Njoo na ujionee mwenyewe. Usisimame nje na kukosoa huko kando kando, Bali, "Thibitisha mambo yote, na ushikilie sana lile lililo jema." Njoo uone.

62 Wakaondoka pamoja wakienda zao njiani, wakizungumza. Alipotembea akafika kwenye uwepo wa Bwana Yesu, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli ambaye ndani yake hamna hila."

63 Karibu limchune ngozi yote. Akaangalia pande zote, akasema, "Vema, Rabi, ulipataje kunijua mimi? Kamwe hujawahi kuniona. Unanijuaje?" Akasema Filipo. . .

64 "Kabla, wakati alipokuita. . ." Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, jana, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona." Amina.

65 Akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

66 Mwanamke mmoja alienda Mbele Zake, Naye akasema, "Nenda, kamwite mumeo."

Akasema, "Sina yeyote."

67 Kasema, "Hiyo ni kweli. Unao watano, na yule mmoja unayeishi naye sasa siye wako. Umesema kweli." Wazia jambo hilo.

68 Akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii. Kwamba, tunajua ya kwamba Masihi atakapokuja atatwambia mambo yote."

69 Akasema, "Mimi Ndiye, ninayesema nawe."

70 Ndipo akakimbia na kuwaambia watu wa jiji, "Njoni, mmwone Mtu aliyeniambia yote niliyotenda. Je! Haimkini huyu kuwa Ndiye Masihi?" Lilinenwa na Bwana.

71 Ni jambo gani lilitukia? Yesu alisema, kabla hajaondoka, "Mambo niyafanyayo, ninyi nanyi mtayafanya." Hilo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mambo niyatendayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya, hata mengi kuliko haya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba." Loo, ninaweza kuwaona walipokuwa wakienda, kila mahali. Marko 16, "Wakaenda kote kote, wakihubiri; Bwana akitenda kazi pamoja nao, akilithibitisha lile Neno."

Na hapa, Paulo, anaelezea jambo lile lile. Yeye alisema ya kwamba I—Injili ilianza kuhubiriwa na Yesu, na ikathibitishwa kwetu na wale waliomsikia. Hilo ndilo Jiwe la Msingi. Loo, Jina la Bwana lihimidiwe! Hilo ndilo Jiwe la Msingi.

72 Na kuwazia, miaka elfu mbili imepita. Wakana Mungu wameinuka, na makafiri, na wenye kushuku, na wasioamini kuna Mungu. Lakini, leo, Yesu huyo huyo anathibitisha Neno Lake katika njia ile ile kwa wale wanaomsikia. "Msikieni Yeye," haimaanishi kusikia tu mahubiri fulani. Hilo linamaanisha, msikieni *Yeye*. Naam.

73 Tutapataje kupona? Kupona kwetu kuko wapi? Loo, unasema, "Mungu atukuzwe, mimi ni mfuasi wa kanisa la Methodisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mpentekoste." Hilo halina uhusiano wowote Nalo. Na kama ukienda pembeni na unataka kuliita "kuwasiliana na mizimu, ama telepathia fulani ya mawazo, ama ibilisi fulani," ama kitu fulani. Aibu kwao!

74 "Kama kila neno la malaika lilikuwa imara . . ." Yesu alisema, "Si ninii . . . Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Na tunapomwona Yeye akishuka, kuendelea kuthibitisha Neno Lake, tutapataje kupona kama tukijipendekeza kwa kanisa fulani, ama shirika fulani, ama madhehebu, ama maskini

nadharia yetu tunayoipenda sana? Afadhali ujiachilie. “Kwa maana kila dhambi ilipokea ujira wa haki chini ya wale malaika, ni zaidi sana vipi wakati Mwana wa Mungu anaponena kutoka Mbinguni, kulidhihirisha Neno Lake! Tutapataje kupona, tusipoujali wokovu mkuu kama huu?” Loo, jamani! “Mungu pia . . .”

Kifungu cha 4:

*Mungu naye akishuhudu pamoja nao . . .*

75 Angalia jambo hili. Bwana alishuhudu. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo! Bwana alishuhudu.

76 Angalia. Wakati Eliya alipoketi juu ya kilima, naye akasema, “Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka Mbinguni ukawateketeze.” Mungu alishuhudu ya kwamba yeye *alikuwa* ni mtu wa Mungu.

Mungu daima hushuhudu. Maisha yako yatashuhudu. Sijui ushuhuda wako ukoje, bali maisha yako yananena kwa sauti kubwa sana, sauti yako haiwezi kusikika. Lakini, mwe—mwenendo wako, maisha yako ya kila siku yatashuhudia kwamba wewe u nani. Mungu hushuhudia. Naam. Roho Mtakatifu ni muhuri, na muhuri huchukua pande zote mbili za karatasi. Wanakuona umesimama *hapa* na wanakuona ukiondoka. Si kanisani tu bali katika kazi ya kila siku. Umetiwa muhuri pande zote mbili, ndani na nje. Kwa furaha uliyo nayo, na kwa maisha unayoishi, umetiwa muhuri, ndani na nje, kwamba unajua umeokoka na ulimwengu unajua umeokoka, kwa maisha unayoishi, kwa maana Mungu anashuhudia. Jina Lake Takatifu litukuzwe! Jamani, ninajisikia wa kiroho!

77 Wazieni jambo hilo, enyi ndugu, pale. Loo! “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu, wala mgeni hawatamfuata.” Loo, jinsi ambavyo majina yetu yako kwenye viganja vya mikono Yake! Yako mbele Zake, mchana na usiku. Neno Lake daima liko mbele Zake, Ahadi Yake. Hawezi kusahau jambo hilo. Naye anakupenda.

78 Sasa, Yeye atawashuhudia walio Wake. Hufungui mdomo wako na kusema neno, ulimwengu utajua jambo fulani limetukia kwako.

. . . kushuhudia *kwa ishara nyingi na maajabu na kwa miujiza ya namna nyingi, na karama za Roho Mtakatifu, kulingana na mapenzi yake?*

79 Hebu na tuchukue tu Andiko moja sasa kabla ya kufunga; kwenye ile Siku ya Pentekoste, wakati walipompokea Roho Mtakatifu. Yapata siku nne baadaye, Petro alikuwa amepitia kwenye mlango uitwao Mzuri; yeye na Yohana. Wakamwambia mtu mmoja, “Tutazame sisi.” Ndipo Petro akasema, “Mimi sina fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nitakachokupa. Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama

na uende." Ndipo huyo mtu akaangalia juu wala kamwe hakuhoji neno lolote kuhusu hilo. Akasimama tu na akaanza kutembea. Walikuwa ni watu wasio na elimu wala maarifa. Lakini Biblia ilisema, "Iliwabidi watambue, kwa kuwa walijua walikuwa pamoja na Yesu.

80 Ndugu, ulimwengu unapojua ya kwamba wewe umekuwa pamoja na Yesu, wakati unapoweza kuishi maisha yasiyoghoshiwa katika ulimwengu huu wa sasa na katika giza hili, ambapo ulimwengu unajua na unaweza kuona ya kwamba wewe umekuwa pamoja na Yesu; wakati maskini kahaba mchafu sana wa barabarani na mjeuri anapoweza kuwa mwanamke wa kuheshimika, ameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo; Mungu anajishuhudia ya kwamba yu hai.

81 Hebu mchukue mlevi, ambaye ni duni sana hata angeweza kuzurura akamwacha mkewe, ambaye angewatesa watoto wake, na kuondoa chakula mezani, apate kutumia fedha na kahaba. Hebu na akutane na Yesu siku moja. Utamwona akirudi, kama yule Jeshi, aliyekuwa na akili zake timamu na amevaa nguo, kwa watoto wake wachanga na kwa mkewe na kwa wapendwa wake. Naam.

82 Hapo zamani siku moja, yapata miaka arobaini iliyopita, wakati dini za ulimwengu zilipokutana, na watu mbali mbali wakasimama na kuzungumza. Pia Mwislamu alizungumza kwa niaba ya dini ya Kiislamu. Wajaini walizungumza kwa niaba ya Wajaini; Mbudha kwa niaba ya Budha. Na maskini yule daktari, ninasahau jina lake la ukoo lilikuwa ni jina gani, sasa hivi tu. Nilijua jina lake, bali nimelisahau. Yeye alizungumza kuwakilisha Ukristo. Ndipo akasimulia hadithi ya Bibi Maccabee wa Oklahoma, Marekani.

Bibi huyo alikuwa mkaidi na malaya kupita kiasi, mpaka hata wakati walipoenda kumwua, wasingeweza hata kumgusa kwa mikono yao, alikuwa mshenzi na mwovu sana. Walikuwa wamemshika kwa shtaka la: kuvuta msokoto; kuendesha gari la farasi; pia alivunja she—she—sheria, ushahidi huko Oklahoma, wakati alipopita mtaani, akiwaendesha farasi wanne wakubwa. Naye alikuwa ameoza kabisa na mchafu sana hata watu wasingeweza kumkaribia; kiasi, mpaka wakati wanyongaji walipokuwa wakienda kumnyonga, wasingemnyonga. Walimmwagia tu lami na manyoya, wapate kumwua.

Ndipo wakati maskini mhubiri huyu aliposimulia juu ya hadithi ya huyo mama, kwa namna fulani, hata aliwafanya watu waketi kwenye pembe za viti vyao, wakisikiliza ni kipi kingefuata. Alipofikia hapo: ameoza kabisa, mchafu, malaya kupindukia, mpaka hata sheria isingeweza kupoteza muda naye, alikuwa ni mshenzi sana. Ibilisi mwenyewe kuzimu angelimkataa mtu kama huyo, jinsi alivyoisimulia hadithi hiyo.

Ndipo akasema, "Waungwana, wa dini za dunia, je! dini yenu ina chochote ambacho kingeweza kuisafisha mikono ya Bibi Maccabee?"

83 Kila mtu aliketi kimya. Ndipo akapiga makofi, na akaruka juu hewani. Akasema, "Utukufu kwa Mungu! Damu ya Yesu Kristo haitaisafisha mikono yake tu, bali itausafisha moyo wake na kumfanya Bibi-arusi Wake." Nakwambia:

Neema ya ajabu! Jinsi inavyosikika tamu,
Iliyomwokoa mnyonge kama mimi!
Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, bali sasa nimepatikana,
Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
Neema ndiyo iliyoondoa hofu yangu;
Jinsi neema hiyo ilivyoonekana ya thamani
Ile saa niliyoamini kwa mara ya kwanza!

84 Bila shaka, "Tutapataje kupona, tusipoujali huo?" Usipojali kula, utakufa. Usipojali kupiga kona, utapata ajali. Usipojali kumkamua ng'ombe maziwa, atakauka. Usipoyajali meno yako, itabidi uyang'oe yote. Bila shaka, utajutia kutojali kwako.

85 Enyi Maskani ya Branham na ninyi wageni, hebu niwaambie jambo fulani sasa. Msipojali kushuhudia utukufu wa Mungu, msipojali kumpa Mungu sifa na utukufu, mtajikuta mkiwa baridi, wa kawaida, na waliorudi nyuma, moja ya siku hizi. Msifuni Mungu. "Tutapataje kupona, tusipoujali wokovu mkuu kama huu?"

86 Tunachelewa. Nilimwona sasa hivi tu, Ndugu Toms alikuwa ameingia kule nyuma. Tutafunga na kuendelea na jambo hili usiku wa leo, Bwana akipenda.

Na tuombe tu kwa muda kidogo.

87 Baba yetu wa Mbinguni, Kwako na ziwe shukrani, na sifa, na heshima, na utukufu, na hekima, na uweza, na nguvu, milele na milele. Loo, kwa huyo Mwana-Kondoo aliyeketi kwenye Kiti cha Enzi, mamlaka na falme na kila kitu viliwekwa mkononi Mwake. Alipofufuka katika wafu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, Yeye alipaaza sauti kwa ulimwengu, "Mamlaka yote Mbinguni na duniani yamewekwa mkononi Mwangu. Enendeni, basi, ulimwenguni kote mkaihubiri Injili."

Ee Mwana-Kondoo mpendwa unayekufa, Damu Yako ya thamani
Kamwe haitapoteza nguvu Zake,
Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

88 Tusaidie, kama wahudumu, kuona ya kwamba sisi ni wahitaji sana; jinsi inavyotupasa kuwa na kanisa, hatuna budi kuwa na *hili*, hatuna budi kuwa na kila kitu.

89 Wanawake wetu, kabla hawajaenda kanisani, wangali wanajiita Wakristo, itawabidi kuwa na nguo ya aina fulani, ama inawabidi kuvalia nadhifu sana.

Na inawabidi wahubiri kuwa na fedha nyingi sana kabla hawajakuja, na kila kitu kinapaswa kuwa *hivi na vile*.

90 Ee Kristo, ninaposoma hapa, "Jinsi walivyozunguka-zunguka, katika ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, wakaishi katika mashimo ya nchi, na mapango." Walizunguka-zunguka, chini ya mateso makali, na, hata hivyo, wakapata Imani, chini ya huduma za malaika. Tutapataje kupona, wakati Bwana Yesu ametupa nyumba nzuri, na magari, na nguo, na chakula? Nasi tunanung'unika. Tunaketi bila shughuli. Tu wavivu. Hatujaribu kamwe kutoka na kufanya jambo fulani. Tutapataje kupona, Mungu?

91 Loo, ninaomba ya kwamba Wewe utawasha moto wa ushawishi wa mtindo wa kale ndani ya kila moyo, asubuhi ya leo, Bwana, ili kwamba watu wapate kuamka na kutenda kazi. Tujalie tufanye kazi wakati nuru ya mchana inamulika, kwa sababu jua linatua haraka sana. Na ustaarabu unakufa, na hapatakuwapo na wakati tena. Utaingia katika Umilele.

92 Ee Mungu, tujalie leo ya kwamba twende tukiwa na ono jipya, tukiwa na hekima, tukiwa na ufahamu, kujua jinsi ya kuwaendea wenye dhambi na kuwaleta kwa Kristo. Yasikie maombi ya mtumishi Wako, Bwana.

93 Naomba, kama kuna mtu yeyote hapa, ambaye hamjui Kristo kama Mwokozi wao, je! ungeweza kuinua mkono wako na kusema, "Nikumbuke, Ndugu Branham"? Ungeweza tu kuinua mkono wako, useme, "Nikumbuke. Ninataka kuwa Mkristo. Sitaki kulipuuza jambo hilo tena"? Mungu akubariki, huko nyuma, bwana. Mtu mwingine? Aseme, "Ninataka kuinua mkono wangu, Ndugu Branham. Nami ninataka kumkubali Kristo, kama Mwokozi wangu, sikujali, muda wote. Loo, ninaenda kanisani, hakika, mimi ni mfuasi wa kanisa."

*Kitabu Cha Waebrania*

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org